OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)
HALMASHAURI YA WILAYA YA MUFINDI

SHULE YA SEKONDARI ITANDULA,
S.L.P 580,
MAKAMBAKO
TAREHE 11/12/2020

Kumb. Na. ITASS/IRA/MUF/JI/2020

JINA LA MWANAFUNZI _____

KIJIJI CHA _____

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA ELIMU YA SEKONDARI KIDATO CHA KWANZA – 2021

1.0. UTANGULIZI

1.1. Nafurahi kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga na masomo ya kidato cha kwanza katika shule ya **Sekondari Itandula.**

1.2. Shule ya **Sekondari Itandula** iko Mkoani **Iringa** katika Wilaya ya **Mufindi**, Tarafa ya **Kasanga**, Kata ya **Itandula,** Kijiji cha **Kimilinzowo**. Shule hii ni ya mchanganyiko (wavulana na wasichana).

1.3. Hali ya hewa iliyopo ni baridi kiasi na ni nzuri kwa masomo.

1.4. Muhula wa kwanza wa masomo utaanza **tarehe 11/01/2021**. Unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe **11/01/2021** saa **1:00 Asubuhi**.

2.0. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

2.1. SARE ZA SHULE

A) I) SARE ZA SHULE KWA WASICHANA

1) Sketi mbili (2) kijani jeshi za marinda ya kawaida (kitambaa kizito) ziwe ndefu kupita magoti.
2) Mashati meupe mawili (2) ya mikono mirefu yasiyoonesha mwili (Transparent)
3) Viatu vyeusi vya kamba jozi/pea mbili (2) (zisiwe boots, viatu vyenye visigino virefu au simples).
4) Soksi nyeupe jozi/pea mbili (2) na kuendelea
5) Hijabu nyeupe isiyo na maua (kwa waislamu)
6) Sweta moja rangi ya kijani jeshi.
7) Raba za michezo

II) MAVAZI YA JIONI (EVENING PREPARATION) NA NGUO ZA SHAMBA (SHAMBA DRESS).

1) Truck suit rangi nyeusi zenye upindo mweupe mikononi na pembeni mwa suruali.
2) Sketi ya damu ya mzee
3) T- shirt rangi ya bluu isiyo na maandishi yoyote.
   NB: Nguo hizi ni muhimu kwa sababu hatuta ruhusu mwanafunzi avae nguo za nyumbani wakati wowote akiwa mazingira ya shule.

B) I) SARE ZA SHULE KWA WAVULANA

1) Suruali mbili (2) za kaki zilizoshonwa vizuri ziwe na marinda mawili na zisiwe nyembamba chini na zivaliwe kiunoni kwa mkanda mweusi.
2) Mashati mawili (2) meupe ya mikono mirefu
3) Viatu vyeusi vya ngozi jozi/pea mbili (2) visivyo na urembo na viwe vya kamba
4) Soksi nyeusi jozi/pea mbili (2).
5) Sweta rangi ya kijani jeshi
6) Raba za michezo

II) MAVAZI YA JIONI (EVENING PREPARATION) NA NGUO ZA SHAMBA (SHAMBA DRESS).

1. Truck suit rangi nyeusi zenye upindo mweupe mikononi na pembeni mwa suruali.
2. T- shirt rangi ya bluu isiyo na maandishi yoyote.
3. Suruali nyeusi mbili (2)
   NB: Nguo hizi ni muhimu kwa sababu hatuta ruhusu mwanafunzi avae nguo za nyumbani wakati wowote akiwa mazingira ya shule.

2.2. VIFAA VYA TAALUMA

i) Daftari tisa (9) kubwa counter book (kwaya two).
ii) Daftari ndogo za kawaida tisa (9) kwa ajili ya majaribio.
iii) Kalamu za wino (pen) za kutosha.
iv) Kalamu za mkaa (pensel)
v) Rula
vi) Mfuko wa kubebea daftari (begi)
vii) File (flat file) la kutunzia kumbukumbu zako

3.0. MASOMO YANAYOFUNDISHWA

Katika shule hii masomo yanayofundishwa ni **Hisabati, Kiswahili, Kiiingereza**, **Uraia, Jiografia, Historia, Elimu ya viumbe (Bailojia), Fizikia, Kemia, Literature In English**. Kwa lengo la kuwalea watoto kiroho kila mwanafunzi atahudhuria vipindi vya dini katika dhehebu lake kwa siku iliyopangwa katika ratiba.

4.0. SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu na 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria namba 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia

miongozo yote inayotolewa na TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa Elimu. Baadhi ya mambo ambayo unatakiwa kuzingatia uwapo shuleni pamoja na:-

a) Heshima kwa viongozi, wazazi, walezi, walimu, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamiii kwa ujumla
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule
c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (Evening preparation)
d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazoagizwa kufanya
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako.
f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi, nywele, mazingira ya shule.
g) Kuvaa sare inayohusika wakati wote uwapo shuleni.
h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote
i) Kutunza mali za umma.

4.1. YAFUATAYO NI MAKOSA AMBAYO BAADA YA KUTHIBITISHWA YANAWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE

1. Wizi
2. Uasherati, ubakaji na ushoga
3. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya
4. Uvutaji bangi
5. Makosa ya jinai
6. Kupiga au kupigana
7. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
8. Kuoa au kuolewa
9. Kudharau Bendera yaTaifa
10. Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule
11. Kutoa mimba
12. Kukataa adhabu kwa makusudi
13. Kugoma, kuchochea na kuongoza kuvuruga amani na usalama wa watu
14. Kuwa na **SIMU** ya mkononi (kumiliki simu) au kuwa na kifaa chochote kinacho husiana na simu. Shule ina simu maalumu ambayo mwanafunzi atatumia kuwasiliana na wazazi.

5.0. VIAMBATISHO MUHIMU

5.1. Pamoja na maelekezo hayo hapo juu nafungasha pia viambatisho hivi ambavyo vinatakiwa kuletwa shuleni siku unayoripoti. Ambavyo ni;-

a) Fomu ya uchunguzi wa afya yako (**Medical Examination**) ambayo inapaswa ijazwe na Mganga wa Hospitali inayotambulika na Serikali.

b) Fomu ya maelezo binafsi ya mwanafunzi itakayojazwa ahadi ya mwanafunzi na mzazi kuhusu kufuata taratibu na maelekezo mbalimbali ya shule

5.2. Tafadhali soma magizo hayo kwa umakini na kuyatekeleza kikamilifu.

5.3. Hakuna gharama yoyote inayotakiwa kulipwa na mzazi/mlezi wakati wa uandikishaji wa mwanafunzi.

5.4. Utalazimika kuja na fomu hii ya maelekezo siku unaporipoti.

KARIBU SANA ITANDULA SEKONDARI

……..

ADRIANO A. NGOLI

MKUU WA SHULE

KIAMBATISHI "A"

KUMBUKUMBU MUHIMU ZA MWANAFUNZI

SHULE YA SEKONDARI ITANDULA S.L.P 580, MAKAMBAKO.

A. MWANAFUNZI NA WAZAZI/WALEZI WAKE

(i) Jina la mwanafunzi …….

(ii) Tarehe ya kuzaliwa……Mahali …….

(iii) Jina la baba……yu hai/amefariki……

(iv) Mahali anapoishi: Kijiji/Mji ……Kata……Tarafa…….

(v) Kazi ya baba…… Namba ya simu……

(vi) Jina la mama……yu hai/amefariki……..

(vii) Mahali anapoishi: Kijiji/mji……Kata……Tarafa……

(viii) Kazi ya mama……namba ya simu…..…….

(ix) Jina la mlezi (ikiwa mtoto hana wazazi) …….

(x) Mahali anapoishi: Kijiji/mji……Kata……Tarafa……

(xi) Kazi ya mlezi …… Namba ya simu …….

AHADI YA MWANAFUNZI KUFUATA SHERIA NA TARATIBU ZA SHULE

Mimi……naahidi kufuata sheria, kanuni na taratibu za shule hii na kutekeleza maagizo yote yatakayotolewa na uongozi wa shule wakati wote nitakaokuwa ndani na nje ya shule.

Sahihi …… Tarehe……..

B. AHADI YA MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI

Mimi…….ambaye ni mzazi/mlezi wa mwanafunzi aliyeweka ahadi yake hapo juu, naahidi kumpatia huduma zote muhimu wakati wote atakapokuwa shuleni. Nitakuwa tayari kusaidiana na uongozi wa shule kufuatilia mahudhurio, nidhamu na maendeleo ya taaluma ya mwanangu kwa kipindi chote atakachokuwepo shuleni. Mwanangu awapo shuleni alelewe katika dini ya ……..Dhehebu la……..

Sahihi…….Tarehe…….

N.B. Fomu hii ijazwe na kupelekwa shuleni siku anayoripoti mwanafunzi

KIAMBATISHI "B"

PRESIDENT'S OFFICE – REGIONAL ADMINSTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
MUFINDI DISTRICT COUNCIL
ITANDULA SECONDARY SCHOOL
MEDICAL EXAMINATION FORM

To be completed by medical Officers in recognize hospital in respect of all new entrants of ITANDULA SECONDARY SCHOOL

Full Name…… Age …….

1. Blood comment (Red & White) ……
2. Pregnancy test (kwa wasichana tu) ……
3. Urine examination……
4. Stool examination……..
5. Syphilis test……..
6. T.B. Test……..
7. Ear Test ……..
8. Spleen ……..
9. Abdominal test…….
10. Eye test ……..
11. Additional information or any other physical, hereditary or infectious disease

    ……

    ……

    Treatment after examination

……

……

MEDICAL CERTIFICATE

I certify that the above mentioned has been examined and found fit to pursue for further education

Signature……

Designation……

Station……

Official stamp…… Date ……

N.B.Fomu hii ijazwe na Mganga katika hospitali inayotambulika na ikabidhiwe kwa mwandikishaji siku ya kuripoti mwanafunzi shuleni.